

Usaidizi na Nyumba baada ya Kunyimwa Madai yako ya Uhamisho na Rufaa zote

Ikiwa Home Office* haijafanya uamuzi juu ya madai yako ya uhamisho, au ikiwa una rufaa zozote zinazoendelea, unaweza kustahiki usaidizi kutoka kwa NASS* Usaidizi wako unaweza kubadilika ikiwa umenyimwa madai yako ya uhamisho na rufaa zote.

Je! Nimenyimwa madai yangu ya uhamisho na rufaa zote?

Ikiwa huna uhakika, au ikiwa hali katika nchi yako ya asili imebadilika, unahitaji kupata ushauri wa kisheria kwa haraka iwezekanavyo - muulize wakili wako akushauri au muulize mfanyakazi orodha ya mawakili.

Usaidizi baada ya kunyimwa madai yako ya uhamisho na rufaa zote

Inaweza kuwa vigumu kupata nyumba au usaidizi baada ya kunyimwa madai yako ya uhamisho. Walakini, kuna chaguzi chache:

1. Sehemu ya 95 ya usaidizi - usaidizi unaopekea wakati wa madai yako ya uhamisho

- Ikiwa una watoto chini ya umri wa miaka 18 ambao wanaishi na wewe kabla ya usaidizi wa NASS* S95 kuisha, kwa kawaida utaendelea hadi watoto wako wote wafike umri wa miaka 18.
- Ikiwa hauna watoto, usaidizi wako wa NASS S95* utasimamishwa siku 21 baada ya kunyimwa uhamisho. NASS* itakujulisha juu ya hii katika barua.

2. Usaidizi wa sehemu ya 4 - nyumba ya kawaida na chakula au vocha.

- Ikiwa una watoto baada ya NASS S95* yako kusimamishwa, au ikiwa hauwezi kutoka Uingereza au ikiwa umeomba kurudi kwa ihari nchini mwako, unaweza kustahiki usaidizi wa Sehemu ya 4. **Tafadhali angalia kijikarata cha Refugee Action's* kuhusu usaidizi wa Section 4* kwa maelezo.**

3. Usaidizi wa Serikali za mitaa

- Ikiwa una shida kali za kimwili/ kiakili au wewe ni mzee/ mgonjwa Local Authority* inaweza kukupatia nyumba na usaidizi. Watahitaji kukuchunguza kwanza - hii inaitwa Community Care Assessment* na inaweza kuchukua wiki chache.
- Ikiwa una watoto na hawastahiki usaidizi wa S95 au S4 Serikali za Mitaa lazima iwasaidie watoto wako lakini inaweza kukataa kumsaidia mtu yeyote katika familia yako aliyezidi umri wa miaka 18.

Ikiwa haufai katika kitengo chochote kilio hapo juu kunaweza kuwa na mashirika ya mtaani ambayo yanaweza kukusaidia kupata nyumba, chakula au mavazi.

Tafadhali muulize mfanyakazi ikiwa una maswali yoyote.

*Maneno haya ni majina ya Kiingereza ya mashirika au maneno mengine ambayo hayawezi kutafsiriwa. Tafadhali muulize mfanyakazi wa ushauri akufafanulie maana yake.